JINA …………………………………………………………………. NAMBARI…………

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
MUDA 2½

.
KIDATO CHA TATU
.

MAAGIZO

Jibu maswali yote

Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali

**Kwa matumizi ya Mtahini**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

## 1. UFAHAMU

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma. Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano, kama maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabdhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti ya kumiliki mashamba, vitambulisho na nyinginezo kwa raia. Kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.
Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya. Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini. Watumishi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari, nyumba na ardh na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyi kazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hosptiali za umma na kupeleka vituo vyao vya afya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umma wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, wahandisi, mawakili, walimu na mahasibu ambao hukwepa majukumu yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi.

Wengine wasio wataalam huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kopokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwingine halazimika kusalimu amri na kutoa hongo ili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa.

Wale wasiojimudu kifedha hubaki wakilia ngoa. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'udugu' kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza hudumia jamii.

Ufisadi umekita mizizi na kushamiri katika sekta za umma na za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyakazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa humjui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyikazi wasiohitimu na wasiowajibika kazini.
Hata hivyo, mbio za sakafuni huishia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi.

Tayari tume kadhaa zimebuniwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni tume ya kuchuguza kashfa ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia zisiso halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo.

Serikali pia imeunda kamati ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi waliohasiriwa na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa kuwalipa au kuwatetea mahakamani ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

**Maswali**

(a) Eleza aina nne za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma (al. 4)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(b) Kulingana na kifungu ulichosoma, ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani? (al. 2)

______________________________________________

______________________________________________

(c) Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi? (al.3)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(d) Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini? (al.2)

______________________________________________

______________________________________________

(e) Toa msamiati mwingine wenye maana sawa na rushwa (al. 1)

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kifunguni. (al.3)

(i) shamiri ______________________________________

(ii) Kashfa ______________________________________

(iii) kita mizizi ___________________________________

## 2. UFUPISHO

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali uliyolizwa**

Uzalishaji wa vyakula popote pale ulimwenguni unahusiana, na labda hata kudhibitiwa, na mazingira ambamo wanaohusika wanaishi. Hata hivyo, jambo la kusikitisha ni kuwa uharibifu wa kimazingira umefikia hatua ya kusikitisha. Uharibifu huo unatokana na amali nyingi za kibinadamu ambazo zinaishia kuwa msingi wa mazingira yake kuathirika. Ikiwa mazingira yameharibiwa kwa jinsi yoyote, kuna athari hasi ambazo hutokea. Kwanza, rutuba iliyoko mchangani inafifia. Kiwango cha mvua kinafifizwa pia na matendo hayo sawa na kuzuka kwa ongezeko la joto. Wataalamu wanaeleza kuwa jangwa la Sahara linapanuka kwa zaidi ya kilometa kumi kwa mwaka. Ikiwa hali hii itaendelea, itachukua miaka michache kwa sehemu kubwa ya bara la Afrika kugubikwa na mchanga wa jangwa hilo. Mgubiko huo utakuwa na matokeo ambayo ni ya kusikitisha.

Yapo maeneo ambako miaka michache iliyopita yalisheheni rutuba namboji lakini sasa hivi hayana uwezo wa kuikuza hii mimea yoyote ile. Zipo njia nyingi ambazo huchangia kwenye tanzo hili la mazingira. Mojawapo katika matatizo hayo ni ukataji wa miti kiholela. Ukataji huu ona athari mbaya hasa pale ambapo kiwango cha miti iliyokatwa au miche inayoatikwa.

Tatizo jingine ni ufugaji unaokiuka uwezo wa kipande cha ardhi cha kuhimili mifugo. Ufugaji wa aina hii unatokana na kupungua kwa malisho yenyewe na labda kwa kiasi Fulani kuendelezwa kwa tamaduni zinazohimiza ufugaji pasi na kuwepo juhudi za kuipunguza mifugo yenyewe. Lipo tatizo linalohusiana na kilimo, yaani ulimaji uliozidi. Ulimaji huu unahusisha upandaji wa-zao lile lile katika ardhi ile ile msimu hadi insimu. Huhusisha pia kilimo kisichotegemea mbolea au samadi. Hali kama hii inaweza kutokana na wakulima kutumia mabua ya mabaki ya chakula kwa ajili ya moto badala ya kuwa nyenzo ya kuundia mbolea.

Kuwepo kwa mazingira kuna mchango mkubwa kwenye lishe ya jamii inayohusika. Kwa mfano, miti na mimea inaweza kuwa chanzo cha rutuba ya udongo. Aidha husaidia kukuzuia udongo usimomonyolewe na maji. Husaidia pia kuhifadhi maji.

Hali kama hii inawezesha kuwepo kwa miti ya matunda kama miembe, michungwa, mitufaa, mipera na kadhalika. Hali hii pia inasaidia kuwepo kwa miti inayozalisha mafuta kama minazi. Mazingira mazuri ni msingi muhimu wa kuwepo kwa majani. Majani haya ni chakula muhimu cha wanyama ambao pia ni chanzo cha chakula kwa wanadamu. Misitu, inayokua katika mazingira ya mvua huwa maskani ya nyuki (wanaoleta asali) na mimea kama uyoga (unaoliwa), Mikoko inayoota karibu na bahari na mazingira mazuri ya kamba na samaki wengine. Isitoshe, miti huwa kuwa chanzo cha kuni za kupikia.

**<u>Maswali</u>**

(a) Kwa kutumia maneno 60 – 65,eleza vile uharibifu wa mazingira kuendelezwa (al.8)
Matayarisho

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

Nakala Safi

(b) Eleza uhusiano uliopo kati ya mazingira na lishe bora (al.7)

Matayarisho

Nakala safi

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

A. Ni nini tofauti kuu kati ya irabu na konsonanti (al.2)

B. (i) Taja sifa bainifu za /e/

(ii) Tofautisha sauti /f/ na (v) ukizingatia namna ya kutamka.

(al.2)

C. Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi (al. 2)

(i) Mighairi

(ii) madhali

D. Tumia visawe vya maneno yafuatayo katika sentensi (al.2)

(i) mwandani

(ii) Nyoka

E. Tunga sentensi kuonyesha matumizi matatu ya ‘ku’ (al.3)

(i)

(ii)

(iii)

F. Tunga sentensi moja ukitumia nomino katika ngeli ya Li-Ya (al.2)

G. Ainisha vitenzi katika sentensi zifuatazo (al.3)

(i) Lenaiyara alikuwa nyumbani

(ii) Lenaiyara alikuwa akilala nyumbani

H. Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa (wingi) (al.2)
Nyumba hiyo ni ya mwanamke wa mzee huyo

I. Andika katika usemi wa taarifa (al.3)
"Kumbuka kuwa lazima ufike mapema kama wataka tuandamane leo". Baba akaniambia.

J. Tambua virai vilivyopigiwa mstari chini (al.2

<u>Mwanafunzi mchafu</u> amefukuzwa <u>shuleni leo</u>

K. Andika sentensi kwa kutumia viambishi vya nyakati na hali zifuatazo (al.4)

(i) a

(ii) ja

L. Taja aina tatu za sentensi na kwa kila mojawapo toa mfano (al.3)
(i)

(ii)

(iii)

M. Tambua shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi (al.2)

Mtoto alisomea mama kitabu

N. Nyambua kitenzi 'fa' katika kauli zifuatazo (al.2)

(i) Tendea ________________________________

(ii) Tendewa ________________________________

O. Eleza matumizi ya 'kwetu' katika sentensi zifuatazo (al.2)

(i) kwetu ni huku

(ii) Mahali kwetu ni huku

P. Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (al.2)

Khalif alisema kwamba lazima afaulu mtihani mwaka huu

Q. Unda vitenzi kutokana na nomino zifuatazo (al.2)

(i) Kinywaji

(ii) hotuba

4. **ISIMU JAMII** (AL. 10)

"Mabibi na Mabwana …………. Kaunti yetu imebaki nyuma kwa sababu ua uongozi duni. Raudi hii wababa na wamama pamoja na vijanaa lazima mabuda maanalogue tuwasend home. Mkinidunga votes zenu nitamake sure ………………..

(a) Tambua sajili iliyotumika (al.2)

(b) Eleza sifa za sajili hii (al.8)